SERA G002: SERA NA TARATIBU ZA ULINZI WA MTOTO

Mhusika: Toleo la sasa limeidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi:	CEO Juni 2023	Toleo: Tarehe ya mapitio yajayo:	2.9 Februari 2028

DIBAJI

Sera hii imeandikwa na So They Can (Shirika la Australia) kwa matumizi katika ofisi zote za So They Can. So They Can inaendesha ofisi sita zilizosajiliwa nchini Australia, Kenya, Tanzania, New Zealand, England & Wales, na Marekani, ambazo ni sehemu ya So They Can Global Alliance. Katika sera hii, 'Mkurugenzi Mtendaji (CEO)' inamaanisha Mkurugenzi Mtendaji wa So They Can (Shirika la Australia). Isipokuwa pale ambapo imeelezwa vinginevyo, 'Bodi' inamaanisha bodi ya So They Can (Shirika la Australia). Sera hii imelenga wafanyakazi wote wa So They Can, wanabodi na wanaojitolea, katika ofisi zote 6 za So They Can. Taratibu za So They Can zinaendana na sera za So They Can.

UTANGULIZI

So They Can ina msimamo wa kutokubali kabisa unyanyasaji na unyonyaji wa aina zote wa watoto na inatekeleza haki za watoto kama zilivyoainishwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (1989).

Watoto wana haki ya kuishi, kukua, kulindwa na kushiriki. So They Can inatekeleza majukumu yake kwa uzito na inalenga kila wakati kuwa na mazingira salama zaidi kwa watoto walioko chini ya uangalizi wake. Itachukua hatua zote zinazowezekana kulinda maslahi, haki na ustawi wa watoto walio katika shirika na itatetea kuimarisha ulinzi na kukuza haki za watoto wote katika jamii. So They Can ina jukumu la kutekeleza kanuni na taratibu zilizoainishwa katika waraka huu ili kulinda watoto dhidi ya unyanyasaji na unyonyaji na Wawakilishi wote wanaofanya kazi au kuwasiliana na watoto. Kufuata sera hii ni sharti la lazima kwa Wawakilishi wote.

So They Can inatambua kuwa ni muhimu kwa wawakilishi wote wa So They Can katika nchi zake za miradi kuwa na ufahamu wa sheria za kulinda watoto za nchi husika na madhara ya kuzivunja. Hivi sasa, kwa kuwa nchi za miradi ya So They Can ni Kenya na Tanzania, sheria hizo ni pamoja na:

- Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto
- Sheria ya Watoto ya 2022 nchini Kenya
- Sheria ya Mtoto nchini Tanzania

UFAFANUZI

- Kwa kuzingatia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto, mtoto katika sera na taratibu hizi anamaanisha mtu yeyote aliye na umri chini ya miaka 18.
- **Wawakilishi wa So They Can** – ni watu binafsi na taasisi zote zinazotenda kwa niaba ya So They Can, bila kujali kama kuna makubaliano rasmi ya kisheria kati yao na So They Can au la.

Hawa wanajumuisha, lakini bila kikomo, wadhamini wote, wanachama, wakurugenzi, wafanyakazi, wenye mikataba, washauri waelekezi, washauri, wanaojitolea, wafanyakazi wa muda mfupi, pamoja na wasambazaji wa kawaida wa bidhaa na huduma, na washirika wa utekelezaji, bila kujali nchi ambako jukumu lao linatekelezwa.

- **Kuwasiliana na watoto**: Kufanya kazi katika shughuli au nafasi inayohusisha au inayoweza kuhusisha mawasiliano na watoto, aidha kulingana na maelezo ya nafasi ya kazi au kulingana na mazingira ya kazi.
- **Kufanya kazi na watoto**: Kufanya kazi na watoto kunamaanisha kushiriki katika shughuli pamoja na mtoto ambapo mawasiliano yanatarajiwa kama sehemu ya kawaida ya shughuli hiyo, na mawasiliano si ya kubahatisha. Kufanya kazi kunajumuisha kujitolea au kazi nyingine zisizo na malipo.
- **Ukaguzi wa rekodi ya uhalifu**: Ni ukaguzi wa historia ya uhalifu ya mtu binafsi unaofanywa na polisi au mamlaka nyingine inayohusika katika kufanya ukaguzi huo. Mhusika anatakiwa kutoa ridhaa kwa ukaguzi wa rekodi ya uhalifu na anapaswa kufahamishwa madhumuni ya matumizi ya cheti cha uthibitisho kutoka polisi kinachoonyesha matokeo ya ukaguzi wa rekodi ya uhalifu.

Unyanyasaji wa Mtoto unajumuisha:

- **Unyanyasaji wa kimwili**: ni matumizi ya nguvu za mwili dhidi ya mtoto yanayosababisha madhara kwa mtoto. Tabia za unyanyasaji wa kimwili zinaweza kujumuisha kumsukuma, kumpiga, kumpiga kofi, kumtingisha, kumtupa, kumpiga ngumi, kumpiga teke, kumng'ata, kumchoma kwa moto, kumnyonga na kumpa sumu.
- **Unyanyasaji wa kingono**: ni mtu mzima, mtoto au kijanabalehe kumtumia mtoto kujiridhisha kingono. Tabia za unyanyasaji wa kingono zinaweza kujumuisha kushika sehemu za siri; kujichua; ngono ya mdomo; kuingiza uume, kidole au kitu chochote katika uke au njia ya haja kubwa; kushika matiti; kuchungulia kwa nia ya kingono; kuonesha uchi; na kumwonesha mtoto au kumhusisha mtoto katika picha za ngono.
- **Unyanyasaji wa kihisia**: unahusu matumizi ya maneno au ishara zisizofaa zinazotumiwa na mzazi au mlezi dhidi ya mtoto, au mwenendo wa muda mrefu wa kushindwa kumpa mtoto malezi toshelevu yasiyo ya kimwili pamoja na kumsaidia kihisia. Matendo hayo yana uwezekano mkubwa wa kuharibu hali ya kujiamini ya mtoto au uwezo wake wa kushirikiana kijamii.
- **Kutelekeza:** ni kushindwa kwa mzazi au mlezi (ikiwa ana uwezo) kumpatia mtoto mazingira na mahitaji ambayo kwa kawaida yanakubalika kuwa ni ya msingi kwa maendeleo ya kimwili na kihisia pamoja na ustawi wa mtoto.
- **Uonevu**: ni kumwadhibu au kumrekebisha mtoto kwa namna isiyo ya busara, isiyofaa au isiyokubalika; kumwekea mtoto masharti makubwa kupita kiasi na/au yanayodhalilisha; kutumia nguvu au chuki dhidi ya mtoto; na/au kuonyesha mwenendo wa mara kwa mara wa maneno au vitendo vya chuki, visivyo vya busara, na vinavyomdhalilisha mtoto.

- **Unyonyaji kwa mtoto** ni miongoni mwa kitendo/vitendo vifuatavyo:

    - Kutekeleza au kumlazimisha mtu mwingine kutekeleza kitendo au vitendo vya unyanyasaji dhidi ya mtoto.

- Kumiliki, kudhibiti, kutengeneza, kusambaza, kupata au kusafirisha/kutuma zana za unyonyaji dhidi ya watoto.
- Kutekeleza au kumlazimisha mtu mwingine kutekeleza kitendo au vitendo vya kumlaghai mtoto ana kwa ana au mtandaoni.
- Kumtumia mtoto kwa faida, kazi, kujiridhisha kingono au kwa manufaa mengine ya binafsi au ya kifedha.

- **Madhara**: Athari yoyote mbaya inayomkumba mtoto katika ustawi wake wa kimwili, kisaikolojia au kihisia. Madhara yanaweza kusababishwa na unyanyasaji wa kifedha, kimwili au kihisia, kutelekezwa, na/au unyanyasaji au unyonyaji wa kingono, iwe kwa makusudi au bila kukusudia.
- **Zana za unyonyaji wa watoto**: Zana yoyote, bila kujali umbo au aina yake, inayotambuliwa kama zana ya unyanyasaji wa watoto au picha za ngono kwa watoto.
- **Zana za unyanyasaji wa watoto**: Zana zinazoonyesha (kwa uwazi au kwa njia isiyo ya moja kwa moja) mtoto kama mwathirika wa mateso, ukatili au unyanyasaji wa kimwili.
- **Zana za ponografia kwa watoto**: Zana zinazoonyesha mtu, au uwakilishi wa mtu, ambaye ni au anaonekana kuwa na umri chini ya miaka 18, akijihusisha au anayeonekana kujihusisha na mkao wa kingono au tendo la kingono, au akiwa katika uwepo wa mtu anayejihusisha au anayeonekana kujihusisha na mkao au tendo la kingono, kwa namna ambayo mtu mwenye akili timamu angeiona, katika mazingira yote, kuwa ni ya kuudhi.
- **Kushawishi**: ni mwenendo unaomrahisishia mkosaji kumpata mtoto kwa ajili ya shughuli za kingono. Kwa mfano, mkosaji anaweza kujenga uhusiano wa kuaminiana na mtoto, kisha kuanza kuupa uhusiano huo mwelekeo wa kingono (kwa mfano kwa kuchochea hisia za kimapenzi au kumwonesha tabia za kingono kupitia ponografia).
- **Kushawishi kimtandao**: ni kitendo cha kutuma ujumbe wa kielektroniki kwa mtoto kwa nia ya kumshawishi apate au akubali kushiriki katika tendo la kingono na mtu mwingine, ikiwamo lakini si lazima iwe mtumaji wa ujumbe; au kutuma ujumbe wa kielektroniki wenye maudhui machafu kwa mpokeaji ambaye mtumaji anaamini kuwa ni mtoto.
- **Mwathirika-mnusurika**: *Mtoto mwathirika-mnusurika* ni neno linalotumika kumwelezea mtu aliye chini ya umri wa miaka 18 ambaye ananyanyaswa, anafanyiwa unyonyaji au amepata madhara, au aliyewahi kupitia hali hizo. Neno *mwathirika-mnusurika* linatambua madhara aliyopata (mwathirika) pamoja na uwezo, uimara au juhudi za mtoto katika kukabiliana na athari za yaliyomtokea (mnusurika). Neno hili linasisitiza mtazamo wa msaada unaozingatia haki za mtoto na kuhifadhi heshima yake katika mchakato mzima wa kuripoti na kuchukua hatua.

KANUNI ZA SERA

Kanuni ya 1: Kutovumilia unyonyaji na unyanyasaji wa watoto

So They Can ina msimamo wa kutovumilia unyonyaji na unyanyasaji wa watoto. Unyonyaji na unyanyasaji wa watoto utasababisha kuchukuliwa hatua za kisheria za jinai, kiraia, na kinidhamu. So They Can haitashirikiana kwa makusudi iwe moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja na mtu yeyote anayehatarisha usalama wa watoto. So They Can hufanya kazi za kupunguza vihatarishi vya unyonyaji na unyanyasaji wa watoto vinavyohusiana na majukumu na programu zake, na hutoa mafunzo kwa wafanyakazi wake na washirika wake kuhusu wajibu wao chini ya sera hii.

Kanuni ya 2: Kuweka Kipaumbele kwa Maslahi Bora ya Mtoto

Nchi zote ambamo So They Can imesajiliwa kama shirika yaani Australia, New Zealand, England & Wales na Marekani pamoja na Kenya na Tanzania ambako shughuli za maendeleo za So They Can zinafanyika, ni wanachama waliosaini Mkataba wa Haki za Mtoto wa Umoja wa Mataifa. So They Can imejizatiti kulinda haki za mtoto na kutekeleza wajibu wa Australia chini ya mkataba huu. Katika hatua zote zinazohusu watoto, maslahi bora ya mtoto yatapewa kipaumbele kwanza. So They Can na washirika wake wanapaswa kuhakikisha kuwa hatua na maamuzi yote yanaweka kipaumbele kwa haki za watoto, usalama na ustawi wao, na yanaongozwa na mkabala wa “kutosababisha madhara”. Ushughulikiaji wa matukio unapaswa kuzingatia athari za kiwewe, kumlenga mtoto, na kuwezesha upatikanaji wa huduma za msaada.

Kanuni ya 3: Kukuza Ujumuishi na Usawa na Kutambua Utofauti

So They Can na washirika wake wanapaswa kuwa wakarimu kwa watoto wote bila kujali hali zao, uwezo wao, jinsia, utambulisho wa kijinsia, mwonekano wa kijinsia, kabila, umri, uhamaji, pamoja na asili zao za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Jitihada lazima zilenge kushughulikia vikwazo vya ushiriki, ulinzi, utoaji wa taarifa na upatikanaji wa msaada, kama vile lugha, usalama, ubaguzi na upatikanaji wa miundombinu na huduma.

Kanuni ya 4: Kuweka Kipaumbele katika Kukinga

So They Can na washirika wake wanapaswa kuwa makini na wenye kuchukua hatua mapema katika kuimarisha usalama wa watoto na kupunguza vihatarishi vinavyowakabili watoto. Hatua za kuwalinda watoto zinapaswa kujumuishwa kikamilifu katika sera, programu, taratibu za ajira, mafunzo ya wafanyakazi na shughuli za kila siku ili kupunguza hatari na kuwalinda watoto, katika mazingira halisi na mtandaoni.

Kanuni ya 5: Kutumia Mkabala wa Kuwawezesha na Ushirikishwaji

So They Can na washirika wake wanapaswa kuwawezesha watoto kuelewa haki zao, kutoa maoni au kueleza matatizo yao, na kushiriki katika maamuzi yanayowahusu kwa njia zinazolingana na umri wao, za hiari na salama. Familia na jamii zinapaswa kushirikishwa kama washirika katika kuimarisha usalama na ustawi wa mtoto, kwa kujenga uaminifu na kuimarisha ushirikiano.

Kanuni ya 6: Kuripoti Matukio ni Lazima

Kuripoti haraka matukio na tatizo lolote la ulinzi wa watoto ndani ya Programu na Miradi ya So They Can ni lazima. Njia za kuripoti na za kushughulikia lazima ziwe wazi, rahisi kufikiwa (ikiwamo kwa watoto) na za usiri. Njia za kuripoti lazima ziweze kuhakikisha kuwa wale wanaotoa taarifa wanalindwa na kwamba matatizo yanashughulikiwa kwa ufanisi, kwa wakati mwafaka na kwa namna inayofaa.

Kanuni ya 7: Kujumuisha Ulinzi wa Watoto Katika Utamaduni na Uongozi wa Taasisi

So They Can na washirika wake wanapaswa kujumuisha masuala ya ulinzi wa watoto katika uongozi, utawala na utamaduni wa taasisi. Utamaduni imara wa ulinzi unahitaji uwajibikaji wazi, kujizatiti kwa viongozi, uwekezaji wa rasilimali, na ukaguzi na uboreshaji endelevu wa sera na taratibu.

Mbinu Inayozingatia Vihatarishi

So They Can inatumia mbinu inayozingatia vihatarishi na yenye mtazamo wa ulinganifu katika ulinzi wa watoto, ikitambua kwamba vigezo kama muktadha, jinsia, rangi, kabila, ulemavu, mwonekano wa kijinsia, hali ya kijamii na kiuchumi, na kutozingatiwa kwa mfumo fulani, vinaweza kuongeza hali hatarishi na kuunda mahitaji maalumu ya ulinzi.

So They Can na washirika wake watafanya tathmini ya vihatarishi vya ulinzi wa watoto katika maeneo yote ambapo miradi itatekelezwa ili kubaini vigezo vikuu vya vihatarishi na kuandaa mipango ya kupunguza vihatarishi kadri iwezekanavyo. Ubainishaji wa vihatarishi vipya, pamoja na ukaguzi wa vihatarishi endelevu, upimaji wake na mikakati ya kupunguza vihatarishi hivi hufanyika mara kwa mara kwa ajili ya So They Can kama taasisi na miradi yake.

Kwa kuwa sehemu kubwa ya shughuli za Programu na Miradi ya So They Can zinahusisha mawasiliano ya moja kwa moja, ya kudumu au ya muhimu na watoto, So They Can na Washirika wake wa Kutekeleza Programu lazima wafuate na kutekeleza Viwango Jumuishii vya Ulinzi wa Watoto kama vilivyoainishwa katika *Viwango vya Ulinzi wa Mtoto Kwa ajili ya Washirika wa DFAT (Kiambatisho G).*

So They Can imejizatiti kusaidia washirika wake wa ngazi za chini kuandaa sera, taratibu na mbinu zinazolingana na Viwango Msingi au Jumuishi vya Ulinzi wa Watoto kulingana na kiwango chao cha mawasiliano na watoto.

WAJIBU CHINI YA SERA HII

Uongozi wa So They Can

So They Can, kupitia wafanyakazi wake wa ngazi ya juu na mameneja, una wajibu wa kuimarisha haki za watoto na kuwa mstari wa mbele katika kuwalinda watoto. Uongozi una jukumu la kutekeleza sera na taratibu hizi na kuzingatia Kanuni ya Maadili inayohusu ulinzi wa watoto (kama ilivyobainishwa hapa chini). Majukumu mahususi yanajumuisha kujenga uelewa kuhusu ulinzi wa watoto, utetezi, taratibu madhubuti za kuajiri na uchunguzi wa waajiriwa, elimu na mafunzo ikiwamo mafunzo msasa ya mara mbili kwa mwaka kwa Wawakilishi wote wenye uhusiano endelevu na So They Can, udhibiti wa udhamini, kushughulikia malalamiko na tuhuma, pamoja na mifumo na masuala ya kiutawala. Wafanyakazi wa ngazi ya juu na mameneja wana wajibu wa kuhimiza matumizi ya ujumbe wa usalama wa watoto katika kazi zao, ikiwamo mawasiliano yanayozingatia usalama wa watoto katika tovuti, vipeperushi, nyaraka za ajira na machapisho mbalimbali ikiwamo nyaraka za uchangishaji fedha, pamoja na kuhakikisha kuwa Wawakilishi wa So They Can wanaelewa kwa uwazi taratibu na muda wa kuripoti matukio ya ulinzi wa watoto. Mameneja katika ngazi zote wana majukumu mahususi ya kusaidia na kuendeleza mifumo inayodumisha mazingira haya salama. Uongozi una jukumu la kuhakikisha kuwa Wawakilishi wote wanaoingia katika uhusiano na So They Can wamesoma, wameelewa na wamekubali kuzingatia Sera hii ya Ulinzi wa Watoto kwa kusaini fomu ya ridhaa (Kiambatisho A). So They Can ina wajibu wa kutoa toleo la Sera hii ya Ulinzi wa Watoto iliyotafsiriwa katika lugha ya eneo husika katika kila nchi inakofanya shughuli zake, na kuhakikisha

kuwa sera hiyo inasomwa kwa Wawakilishi wote wasiojua kusoma na kuandika kwa lugha wanayoielewa.

Wawakilishi wote

Wawakilishi wote wana wajibu wa kuunda na kudumisha mazingira yanayozuia unyonyaji na aina zote za unyanyasaji na unyonyaji wa watoto, na yanayokuza mwenendo chanya wa wafanyakazi. Wawakilishi wote wanawajibika kuwa na uelewa wa kina wa sera na taratibu hizi, kuchukua hatua kwa kuzingatia sera hizo, na kuzingatia Kanuni ya Maadili ya Wafanyakazi wa So They Can.

TARATIBU

1. Programu za Maendeleo

Watoto katika nchi zinazoendelea wako katika hatari kubwa ya kukabiliwa na aina mbalimbali za unyanyasaji na unyonyaji hasa kutelekezwa, unyanyasaji wa kimwili na wa kihisia. Hivyo basi, kazi za programu za So They Can katika nchi zinazoendelea zinalenga kuimarisha ulinzi wa watoto na kulinda haki za watoto kama sehemu ya msingi ya shughuli zote za programu. Programu zitalenga kufanya kazi moja kwa moja na kwa njia zisizo za moja kwa moja ili kupunguza vihatarishi vinavyowakabili watoto, ziwe zinatoka nje ya familia au ndani ya familia, na shughuli hizi zitapimwa kupitia mchakato wa ufuatiliaji na tathmini. Wawakilishi watapokea mafunzo endelevu na kutaarifiwa mara kwa mara kuhusu masuala yanayohusiana na ulinzi wa watoto.

Wakati wa kufanya kazi na washirika wowote, So They Can itahakikisha kuwa ulinzi wa watoto ni kanuni ya msingi na ya lazima katika kazi za mshirika husika. So They Can itahakikisha kuwa washirika wote wana sera za ulinzi wa watoto zinazozingatia Azimio la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, na kwamba sera hizo zinazingatiwa na kufuatiliwa. Aidha, So They Can itahakikisha kuwa makubaliano yote ya ushirikiano yanajumuisha vifungu maalumu vya ulinzi wa watoto.

2. Kanuni ya Maadili ya Ulinzi wa Mtoto

2.1 Utangulizi

Wawakilishi wote watatenda kwa njia inayokuza haki za watoto na kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji na unyonyaji. Kanuni ya Maadili ya Ulinzi wa Watoto ya So They Can (Kiambatisho A) inaeleza matarajio ya msingi ya Wawakilishi kuhusu mawasiliano na uhusiano wao na watoto.

Watoto wako katika vihatarishi vya unyanyasaji na unyonyaji kutoka vyanzo mbalimbali. Ni wajibu wa Wawakilishi wote kupunguza vihatarishi hivi kwa kuwa mfano mzuri, kubaini na kudhibiti vihatarishi vinavyoweza kujitokeza, na kuchukua hatua stahiki pale tuhuma za unyanyasaji au unyonyaji zinaporipotiwa.

Ukiukwaji wa Kanuni ya Maadili au wa Sera ya Ulinzi wa Watoto ya So They Can ni msingi

wa kuchukuliwa hatua za kinidhamu, unaweza kusababisha kufukuzwa kazini au kusitishwa kwa huduma, na pia unaweza kusababisha kuchukuliwa kwa hatua za kisheria. Ukiukwaji wa kanuni yoyote kati ya kanuni zilizomo katika sera hii utachukuliwa kama kosa kubwa la kinidhamu na utasababisha kufukuzwa au kusitishwa kwa huduma.

3.2. Wajibu wa Kisheria

So They Can inahitaji Wawakilishi wote wazingatie sheria zote zinazohusika (ikiwamo sheria za ulinzi wa watoto).

3. Kuajiri

3.1 Mchakato wa Usaili, Uteuzi na Kuajiri

- Dhamira ya So They Can katika kulinda watoto inaoneshwa kupitia miongozo madhubuti inayohusu kuajiri na uchunguzi unaozingatia usalama wa watoto kwa Wawakilishi, hususan wale watakaokuwa na mawasiliano ya moja kwa moja au kufanya kazi na watoto. Kupitia kuimarisha taratibu za kuajiri na uchunguzi unaozingatia usalama wa watoto, So They Can inapunguza vihatarishi vya kuajiri au kushirikisha mtu anayewanyanyasa au kuwanyonya watoto, na huvutia watu bora zaidi wa kufanya kazi na watoto.
- So They Can ina maelezo ya kazi yaliyo wazi kwa nafasi zote za kazi. Maelezo haya yanajumuisha ujumbe unaozingatia usalama wa watoto pamoja na matarajio chini ya sera ya ulinzi wa watoto na Kanuni ya Maadili ya taasisi. Vigezo vya uteuzi vilivyoainishwa katika maelezo ya kazi vinaeleza uzoefu husika unaohitajika endapo kazi inahusisha kufanya kazi na watoto, na maelezo ya kazi huwafahamisha waombaji kuhusu taratibu za uchunguzi wa kuajiri unaozingatia usalama wa watoto zitakazotumika kwa nafasi zinazohitaji mawasiliano au kufanya kazi na watoto.
- Matangazo yote ya nafasi za kazi yanajumuisha ujumbe unaoonesha kuwa So They Can ni taasisi inayozingatia usalama wa watoto na kuwataarifu wanaoomba kazi kwamba:

    - Uchunguzi wa rekodi za uhalifu utatekelezwa kwa waombaji waliofanikiwa.
    - Uchunguzi wa rekodi za uhalifu unahusisha nchi zote za uraia na kila nchi ambayo mtu amekaa kwa miezi 12 au zaidi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (au zaidi).
    - Masharti ya kufanya uchunguzi wa rekodi za uhalifu yanawapa watu fursa ya kujiondoa wenyewe katika mchakato wa uteuzi.

- Mchakato wa Usaili kwa kazi wa So They Can

- Kujumuisha maswali yanayozingatia usalama wa watoto katika mahojiano kwa kazi zote zinazohusisha watoto (ikijumuisha wafanyakazi waliopo ndani ya taasisi wanaoomba nafasi za ndani, pamoja na wafanyakazi na washauri waliopendekezwa na taasisi nyingine).
- Usaili kufanywa na jopo lenye wanajopo 3–4 badala ya mtu mmoja.
- Kuzingatia kujumuisha kijana kwenye jopo la usaili kwa nafasi zinazohusisha kazi ya moja kwa moja na watoto.
- Kujadili na wanajopo wengine tatizo lolote lililoibuka wakati wa usaili na kufuatilia kwa wadhamini.
- Ikiwezekana, kuepuka kufanya usaili kwa simu au mtandaoni kwa nafasi zinazohusisha kazi ya moja kwa moja na endelevu na watoto. Usaili wa ana kwa ana unatoa fursa bora zaidi ya:
    - Kufahamu tabia ya mtu
    - Kutambua ishara zozote hatarishi au wasiwasi
    - Kutazama lugha ya mwili, mawasiliano ya macho, jinsi anavyowasiliana na waliopo kwenye usaili, pamoja na kusita au dalili zozote za kutofurahia maswali yaliyoulizwa.

- Kutuma sera ya ulinzi wa watoto na Kanuni ya Maadili kwa waombaji kabla ya usaili.
- Kuuliza maswali yanayotoa mwangaza kuhusu mitazamo ya mtu kuhusu watoto, maadili yake, imani na motisha yake (maswali yanayojikita katika tabia).
- Kuuliza maswali yanayojiegemeza katika tukio ili kuchunguza tabia za awali na jinsi mtu alivyoshughulikia baadhi ya matukio fulani.

- Wafanyakazi wote wanaoajiriwa, iwe ndani ya nchi au kutoka nje ya nchi, ambao watafanya kazi kwenye miradi nchini lazima pia wawe na angalau wadhamini mawili ambao taasisi itawasiliana nao.

- Lazima kufanyike mawasiliano ya moja kwa moja na wadhamini na utambulisho wao pamoja na uhusiano wao na mwombaji wa kazi ubainishwe. Maswali yanayohusiana moja kwa moja na ulinzi wa watoto na usalama wa watoto lazima yajumuishwe katika mazungumzo na mdhamini.
- Wawakilishi wote wanapaswa kufahamishwa kuhusu Sera na Taratibu za Ulinzi wa Watoto za So They Can wakati wa mafunzo elekezi ya mazingira ya kazi. Lazima wasaini uthibitisho kwamba wamesoma nyaraka hiyo na watazingatia masharti yake.
- Ufuatiliaji endelevu wa mwombaji kazi anayependekezwa unapaswa kuendelea katika kipindi chote cha mafunzo ya maelekezo ya kazi na katika kipindi cha majaribio ya kazi.

3.2 Uchunguzi wa Rekodi ya Uhalifu

- Uchunguzi wa Rekodi za Uhalifu unaofanywa na Shirikisho la Polisi la Australia (*Australian Federal Police*) utatekelezwa kwa wawakilishi wote raia wa Australia na kwa raia wengine ambao wataajiriwa Australia ambapo nafasi yao ya kazi itahusisha kuwasiliana na/au kufanya kazi na watoto.
- Uchunguzi wa Rekodi za Uhalifu unaofanywa na Polisi wa New Zealand utatekelezwa kwa wawakilishi wote raia wa New Zealand na kwa raia wengine ambao wataajiriwa New Zealand ambapo nafasi yao ya kazi itahusisha kuwasiliana na /au kufanya kazi na watoto.
- Uchunguzi wa Rekodi za Uhalifu unaofanywa na Idara ya Huduma za Taarifa za Haki za Jinai ya FBI utatekelezwa kwa wawakilishi wote raia wa Marekani na kwa raia wengine ambao wataajiriwa Marekani ambapo nafasi yao ya kazi itawahusisha kuwasiliana na /au kufanya kazi na watoto.
- Katika nchi za programu za So They Can, uchunguzi wa rekodi za uhalifu au mfumo mwingine wa kisheria wa uchunguzi ikiwa upo utatekelezwa kwa wawakilishi wote wanaoajiriwa au kupewa mkataba bila kujali jukumu lao. Ikiwa mtu huyo amekuwa akiishi nje ya nchi na kazi yake na So They Can itahusisha kufanya kazi na watoto katika nchi za programu, uchunguzi wa rekodi za uhalifu lazima ufanyike kwa kila nchi aliyokuwa akiishi kwa miezi 12 au zaidi katika miaka mitano iliyopita, pamoja na nchi yake ya uraia.
- Ukaguzi huu utatekelezwa kabla ya kuajiriwa au kuanzishwa kwa uhusiano na So They Can, na ukaguzi wa marudio utafanyika kila baada ya miaka 2 kwa wafanyakazi wote. So They Can haitaajiri au kutoa mkataba kwa mtu aliyehukumiwa kwa kosa linalohusiana na mtoto, au kuruhusu mtu kufanya kazi na watoto ikiwa anatishia usalama wa watoto.
- Meneja wa Nchi/Meneja Rasilimali Watu ana jukumu la kuhakikisha kuwa Wawakilishi wote wana ukaguzi wa rekodi za uhalifu za sasa unaofanyika kila baada ya miaka 2 na kudumisha Rejista ya Ukaguzi wa Rekodi za Uhalifu
- Muhtasari wa masharti ya uchunguzi wa ulinzi wa watoto wa So They Can unawezapatikana katika jedwali lililoambatishwa katika waraka huu (angalia Kiambatisho F).

4. Mafunzo na Maendeleo

Kama sehemu ya mchakato wa kuanza kazi, Wawakilishi wote watapewa nakala ya Sera ya Ulinzi wa Watoto na Kanuni ya Maadili ya So They Can na wataombwa kuisoma na kusaini tamko linalothibitisha kuwa wameielewa na wanakubali kufungwa nayo. Mafunzo msasa kuhusu Sera ya Ulinzi wa Watoto ya So They Can hutolewa kwa wafanyakazi wote katika nchi zinazotekeleza programu mara mbili kwa mwaka, na pia katika vitengo vingine vya So They Can.

Katika nchi zinazotekeleza programu, Mameneja wa Programu na Wasimamizi wa Miradi wana wajibu wa kuhakikisha kuwa wawakilishi walioko chini ya mamlaka yao wanaelewa maudhui ya nyaraka ya Sera na Taratibu za Ulinzi wa Watoto, na wanafahamu sheria za ndani za ulinzi wa watoto pamoja na madhara ya kuzivunja. Hii inaweza kuhusisha tafsiri ya nyaraka husika na maelezo ya ana kwa ana inapohitajika. Mameneja wa Nchi wana wajibu wa kuhakikisha kuwa Mameneja wao wa Programu wanaendesha mafunzo kuhusu Sera ya Ulinzi wa Watoto na Kanuni ya Maadili.

Afisa Mwendeshaji Mkuu wa So They Can ana wajibu wa kuhakikisha kuwa mafunzo ya Sera ya

Ulinzi wa Watoto yanatolewa mara kwa mara katika vitengo vingine vya So They Can.

Mafunzo ya ziada na endelevu ya ulinzi wa watoto yanayohusiana moja kwa moja na majukumu ya kazi yataandaliwa na Mameneja wa Programu kwa Wawakilishi wa So They Can wanaowasiliana au kufanya kazi na watoto. Msimamizi wa Mradi atahakikisha kuwa mafunzo haya yanafanyika na yanaendelea kama inavyotakiwa. Mameneja wa Programu, au Afisa Mwendeshaji Mkuu, watarekodi mafunzo yaliyotolewa kwa kila Mwakilishi katika Rejista ya Mafunzo ya Sera.

5. Masoko na mawasiliano

So They Can itachukua tahadhari zote zinazotakiwa kulinda taarifa za watoto zilizoko katika nakala ngumu na za kielektroniki zilizo chini ya uangalizi wake. Taarifa za watoto zitahifadhiwa katika maeneo salama, na zitapatikana tu kwa watu wa So They Can wanaohitaji taarifa hizo ili kutekeleza majukumu yao.

Hakuna nyaraka za picha, kielektroniki au zilizochapishwa zenye picha au taarifa zinazohusiana na watoto ambazo zinaweza kumweka mtoto katika hatari ya kutambulika zitakazotolewa au kusambazwa kupitia njia yoyote ya mawasiliano bila kuwapo miongozo madhubuti kuhusu matumizi yake.

Picha zote za watoto zinazotumika katika nyaraka za utangazaji au uhamasishaji hazitaambatanishwa na taarifa kuhusu mahali mtoto anapoishi. Maandishi yoyote yanayoambatana na picha ambayo kwa namna yoyote yanamtambulisha mtoto yatafichwa au kuondolewa, isipokuwa pale idhini itakapokuwa imetolewa na Mtendaji Mkuu wa So They Can.

Mpiga picha huru yeyote anayefanya ziara katika miradi ya So They Can, ambako kuna kazi au mawasiliano yanayohusisha watoto, atalazimika kwanza kusoma Sera ya Ulinzi wa Watoto na Kanuni ya Maadili ya So They Can na kujizatiti kuzingatia masharti yake kwa kusaini tamko husika.
Mawasiliano yote yanayohusisha watoto yatatumia picha na maandishi yenye staha na heshima. Katika mawasiliano yote, watoto watakuwa wamevaa ipasavyo kulingana na mila na desturi za eneo husika, na miendo au mikao yoyote inayoweza kuashiria maudhui ya kingono itaepukwa kabisa.

So They Can imeandaa seti ya Miongozo ya Upigaji Picha wa Kimaadili (Kiambatisho D) ili kuhakikisha kuwa picha zote, video na ujumbe wa maandishi unaotumika katika mawasiliano unaonesha watu kwa namna inayoheshimu haki zao, usalama, utu, maadili, historia, dini, lugha na utamaduni wao.

6. Utoaji taarifa na usimamizi wa tuhuma

Uanzishaji, utekelezaji na ufuatiliaji endelevu wa mfumo madhubuti wa usimamizi wa

tuhuma na matukio ni jambo la msingi katika jitihada za So They Can za kuwalinda watoto dhidi ya aina zote za unyanyasaji na unyonyaji, na kuhakikisha haki ya kufuata taratibu kwa wawakilishi wowote wanaohusishwa katika tuhuma.

So They Can inatambua uwezekano wa wawakilishi kutafuta njia ya kupata fursa ya kuwafikia watoto kwa nia za unyanyasaji. Tishio hili linazingatiwa kwa uzito na umakini wa hali ya juu, na So They Can imejizatiti kufanya kila iwezalo kuzuia unyanyasaji na unyonyaji wa watoto, pamoja na kuwawajibisha wale wote wanaowadhuru watoto.

6.1 Wajibu wa Kuripoti Haraka Matukio Yanayoshukiwa ya Unyanyasaji na Unyonyaji

Tukio au tatizo lolote linalohusu usalama au ustawi wa mtoto au watoto wanaohudhuria programu ya So They Can lazima uripotiwe siku hiyohiyo, au siku inayofuata iwapo tukio au tatizo hilo limetokea baada ya saa za kazi. Kutochukua hatua za ulinzi wa mtoto kunaweza kumaanisha kuwa mtoto hajalindwa na anaendelea kuwa katika hatari ya unyanyasaji na unyonyaji zaidi. Hali hii pia inaweza kusababisha kuongezeka kwa waathirika wengine watoto. Vilevile, ni muhimu kufuata ipasavyo taratibu sahihi za kuripoti na kuchukua hatua; ushughulikiaji usiofaa unaweza kusababisha madhara zaidi kwa mtoto.

Wawakilishi wanaweza kuwasilisha tatizo lao kwa maneno, kwa maandishi, au kupitia jukwaa la mtandaoni lisilobainisha jina la Whispli linalopatikana kwa wawakilishi wote. Ikiwa mtu kwa makusudi ataamua kutotoa taarifa ya tukio, basi atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwamo uwezekano wa kufutwa kazi, kusitishiwa mkataba au huduma.
Tukio lolote linaloshukiwa au tuhuma yoyote ya unyonyaji, unyanyasaji au kutokufuata sera kwa mtu yeyote anayewajibika katika sera hii, likihusiana na majukumu rasmi au biashara, lazima liripotiwe kwa Kitengo cha Kanuni na Maadili cha DFAT. Ripoti zote zinapaswa kutumwa kwa baruapepe **childprotection@dfat.gov.au** kwa kutumia fomu ya Taarifa ya Tukio la Ulinzi wa Mtoto (Kiambatisho E). Taarifa zote zinazotolewa zitashughulikiwa kwa mujibu wa sheria husika, ikiwamo Sheria ya Usiri wa Taarifa ya mwaka 1988.

Pale inapowezekana, matukio yanapaswa kuripotiwa kwa kutumia fomu ya Taarifa ya Ulinzi wa Mtoto (Kiambatisho E) na yanapaswa kujumuisha, lakini bila kikomo:

- Ishara maalum (alama yoyote, ugonjwa, jeraha au mabadiliko ya tabia yanayoashiria uwezekano wa unyanyasaji au unyonyaji) kutoka kwa mtoto kuwa ananyanyaswa au kutoa sababu za kuashiria kwamba yeye au mtoto mwingine ananyanyaswa.
- Taarifa kutoka kwa mtu aliyeshuhudia au anayeonesha wasiwasi kuhusu unyanyasaji wa mtoto.

- Ishara yoyote, ugonjwa, jeraha au tabia inayoonesha uwezekano wa unyanyasaji au inayotia wasiwasi au shaka.
- Dalili, jeraha au tabia ambayo haioneshi unyanyasaji moja kwa moja, lakini ikijumuishwa na taarifa au ushahidi mwingine inatoa sababu ya kuwa na wasiwasi.
- Unyanyasaji wa mtoto kwa mtoto: Mtoto aliye katika familia ya So They Can au anayehudhuria programu nyingine yoyote ya So They Can (k.m., programu ya kuimarisha familia) ananyanyasa mtoto mwingine au ananyanyaswa na mtoto mwingine.
- Kuona au kusikia kuhusu unyanyasaji katika taasisi nyingine au katika jamii ambayo So They Can inafanya kazi.
- Kitu chochote kinachoashiria kuwa mfanyakazi au mshirika amenyanyasa mtoto au kumweka mtoto katika kihatarishi cha unyanyasaji au unyonyaji.
- Tuhuma, wasiwasi au uvumi unaoashiria kuwa mfanyakazi au mshirika amekiuka sera ya ulinzi wa mtoto ya So They Can na mwenenndo wa tabia kama ilivyobainishwa katika sehemu ya Kanuni ya Maadili.
- Mtu mzima anaripoti kuwa alinyanyaswa akiwa mtoto au kijana wakati akiwa na mawasiliano na So They Can.

6.2 Hatua za Kinidhamu

Hatua za haraka zinahitajika mara tu tuhuma au tatizo linaporipotiwa ili kuhakikisha kwamba mahitaji ya kiafya na kiusalama ya mtoto au watoto yanatimizwa.

Ndani ya saa 24 tangu tuhuma au tatizo kuripotiwa, timu inayoshiriki katika mchakato wa usimamizi wa tukio lazima ibainishe aina ya tatizo. Meneja wa Nchi na/au meneja aliyeteuliwa ndiye anayeamua hatua zinazofuata. Hatua za mwanzo za kutoa majibu sahihi lazima zichukuliwe ndani ya saa 48 tangu tuhuma au tatizo kuripotiwa, kulingana na hali ya tukio kama ilivyoamuliwa katika kikao cha rufaa.
Kuna machaguo mbalimbali kwa So They Can katika kushughulikia matokeo ya unyanyasaji wa watoto, yakiwamo lakini bila kikomo kwa:

- Wafanyakazi – hatua za kinidhamu / kuondolewa kazini
- Washirika –kusitishwa kwa ushirikiano
- Wenye mikataba – kuvunjwa kwa mkataba
- Kuwasilisha tatizo kwa mamlaka za kitaifa

6.3 Utaratibu wa kuripoti

Matuko au tuhumza zozote za unyanyasaji au udhalilishaji wa mtoto, ikiwa ni pamoja na matumizi yasiyofaa ya nyaraka zilizochapishwa (zamani au sasa) na mwakilishi, lazima ziripotiwe kwa meneja anayehusika siku hiyohiyo, au siku inayofuata ikiwa tukio lililotajwa limetokea baada ya muda wa kazi kwa kutumia Fomu ya Taarifa ya Tukio la Ulinzi wa Mtoto (Kiambatanisho E). Ikiwa hili haliwezekani, basi suala hilo lazima

liripotiwe ndani ya saa 12 zinazofuata kwa meneja wake wa juu, huku kukiwa na uchaguzi wa kuripoti moja kwa moja kwa Mkurugenzi Mtendaji. Mtu anayewasilisha tuhuma anatakiwa, haraka iwezekanavyo (kwa kawaida ndani ya saa 24), kuandika taarifa ya tuhuma hiyo, ikijumuisha muda, mahali na mashahidi wowote.

Tukio au tuhuma zozote za udhalilishaji wa watoto, unyanyasaji au kutokufuata sera kwa mtu yeyote anayewajibika kwa sera hii, zinazohusiana na majukumu rasmi au biashara, lazima ziripotiwe kwa Kitengo cha Maadili na Tabia cha DFAT. Taarifa zote zinapaswa kutumwa kwa childprotection@dfat.gov.au kwa kutumia Fomu ya Taarifa ya Tukio la Ulinzi wa Mtoto (Kiambatanisho E). Taarifa zote zilizotolewa zitashughulikiwa kwa mujibu wa sheria husika, ikiwa ni pamoja na Sheria ya Usiri ya mwaka 1988.

Fomu ya Taarifa ya Tukio pamoja na nyaraka zozote zinazohusiana na tukio, uchunguzi na hitimisho zitahifadhiwa katika Rejista ya Matukio za kila nchi.

Ikiwa anayewasilisha tuhuma ni mtoto, atapelekwa na kusaidiwa na Ofisa wa Msaada wa Mtoto anayehusika, na nyaraka zote zitakamilishwa kwa mujibu wa sera ya malalamiko na masharti yaliyomo ndani ya sera hii. Nchini Tanzania, jukumu la Ofisa wa Msaada wa Mtoto linatekelezwa na Meneja wa Elimu wa So They Can, na ikiwa malalamiko yaliyowasilishwa yanamhusu Meneja wa Elimu, jukumu hilo linatekelezwa na Meneja wa Nchi. Nchini Kenya, mmojawapo wa Wafanyakazi wa Kijamii anateuliwa kutekeleza jukumu la Afisa wa Msaada wa Mtoto.

Ofisa wa Msaada wa Mtoto atakamilisha nyaraka zote na kuwasilisha tuhuma hizo kwa Msimamizi wa Mradi wa eneo husika siku hiyohiyo, au siku inayofuata ikiwa tukio lilitokea baada ya muda wa kazi, na pia kwa Mkurugenzi Mtendaji ndani ya saa 12 zinazofuata. Afisa wa Msaada wa Mtoto atatafuta msaada wa kitaalamu kwa mtoto kama inavyotakiwa. Watoto wote wanapaswa kufahamishwa kupitia Ofisa wao wa Msaada wa Mtoto kuhusu kuwapo kwa njia hii ya kuwasilisha malalamiko na tuhuma dhidi ya wafanyakazi na Wawakilishi wa So They Can, wenzao na wanajamii wengine.

Ikiwa tuhuma zinamhusu meneja wa mtu anayewasilisha tuhuma, basi jambo hilo lazima liripotiwe haraka kwa Mkurugenzi Mtendaji. Iwapo madai yanamhusu Mkurugenzi Mtendaji, basi jambo hilo lazima liripotiwe haraka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya So They Can. Ikiwa tuhuma zinamhusu Mwenyekiti wa Bodi ya So They Can, basi tuhuma ziripotiwe kwa Wakurugenzi wengine wawili wa So They Can.

Wakati wote, So They Can itachukua hatua zinazojali maslahi bora ya mtoto. Hii inaweza kujumuisha kusitisha mara moja au kuhamishia mshukiwa katika jukumu lingine hadi uchunguzi ukamilike. Kila mwakilishi ambaye amesimamishwa kazi atakuwa na haki ya kufahamu mchakato kwa haki na usawa ikiwamo taarifa zinazofaa kuhusu mchakato wa uchunguzi. Hakutakuwa na kukisia kuhusu hatia au usafi wa mtu, huku mchakato wa uchunguzi ukiendelea kuwa wa siri hadi uamuzi utolewe na uongozi. Bila kujali uamuzi

uliofanywa, mchakato lazima uandikwe na kuhifadhiwa, na nyaraka zote zilizochapishwa na za kielektroniki zinapaswa kutunzwa katika mahali salama na pa siri kila wakati.

Meneja, au ikiwa ni lazima Mkurugenzi Mtendaji, ana jukumu la kuchukua hatua zinazofaa ikiwamo:

- Kuchukua hatua za haraka kuhakikisha usalama na ustawi wa mtoto au watoto waliohusika;
- Kutuma ripoti kwa mamlaka za kisheria za eneo husika pale inapofaa;
- Kufuata sheria, kanuni na taratibu husika na kushirikiana na mamlaka za eneo husika;
- Kuamua ikiwa ni sahihi na inawezekana kuwasilisha taarifa kwa Shirikisho la Polisi Australia**,** Polisi wa New Zealand**,** Idara ya Haki ya Taarifa za Uhalifu ya FBI au mamlaka nyingine za kimataifa; na
- Kufanya au kupanga uchunguzi wa ndani ili kubaini kama Sera ya Ulinzi wa Watoto ya So They Can imekiukwa.

Baada ya mchakato wa uchunguzi, Mkurugenzi Mtendaji ataamua mojawapo ya yafuatayo:

- Kuna msingi wa kuanzishwa kwa taratibu za kisheria au kimahakama na Sera na Taratibu za Ulinzi wa Watoto za So They Can zimekiukwa. Katika muktadha huu, suala hilo litawasilishwa kwa mamlaka husika na hatua za kinidhamu, ikiwamo kuondolewa kazini au kusitisha mkataba, zitachukuliwa;
- Hakuna msingi wa kunzisha taraibu za kisheria na kimahakama, lakini mfanyakazi amekiuka Sera ya Ulinzi wa Watoto ya So They Can. Hatua za kinidhamu zitatekelezwa ikiwamo uwezekano kuondolewa kazini au kuvunja mkataba; au
- Hakuna msingi tuhuma hizo, ambapo mtu huyo atarudi kwenye majukumu yake ya kawaida. Ikiwa itagundulika kuwa tuhuma hizo zilikuwa za kiuochezi au udanganyifu, hatua stahiki zitachukuliwa dhidi ya mtu aliyewasilisha tuhuma.

Iwapo jambo hilo litakuwa sehemu ya uchunguzi wa kisheria, So They Can itashirikiana kikamilifu na mamlaka husika.

6.4 Usiri

Matukio na madai yoyote ya unyanyasaji, madhara au unyonyaji wa mtoto hushughulikiwa kwa uangalifu mkubwa na kwa siri. So They Can inaelewa, katika baadhi ya mazingira kuripoti matukio na tuhuma kunaweza kufanyika hata kama mtoto au pande zinazohusika hawataki kutoa ridhaa yao, wakati wote So They Can itafanya kazi kwa maslahi bora ya mtoto. Tatizo lolote litakalojitokeza daima litashughulikiwa kwa kufuata utaratibu rasmi ulioelezwa hapo juu.

Nyaraka zote za tuhuma zozote zilizowasilishwa, iwe kielektroniki au kwa nakala

ngumu (karatasi), zinapaswa kuhifadhiwa mahali salama kila wakati.

NYARAKA ZINAZOHUSIANA

- Sera na Rejista ya Mwongozo wa So They Can
- Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto
- Itifaki ya Hiari ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto
- Sheria ya Makosa ya Jinai ya Jumuiya ya Madola, 1995
- Sera ya Ulinzi wa Watoto ya DFAT (Septemba 2025)

Tarehe	Toleo	Maoni
Juni 2014	1.0	
5 Aprili 2018	2.0	Mapitio ya sera kwa kuzingatia matakwa ya DFAT
17 Desemba 2018	2.1	Kuandaa upya tamko la uzingatiaji wa masharti, mapitio ya taratibu za ajira na uchunguzi, pamoja na Kanuni ya Maadili zinazojitegemea.
Februari 2019	2.2	Mamlaka ya kutoa idhini ya mwisho imebadilishwa kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji (CEO) kwenda kwa Bodi, pamoja na marekebisho ya Miongozo ya Upigaji Picha wa Kimaadili.
Novemba 2019	2.3	Nyongeza ya ufafanuzi wa Ofisa wa Ulinzi wa Mtoto kwa Australia na katika nchi zinazotekeleza miradi.
Desemba2019	2.4	Maelezo ya kina zaidi yameongezwa kuhusu muda wa ukomo wa kuripoti matukio ya ulinzi wa mtoto au tuhuma za matukio hayo.
Oktoba 2020	2.5	Nyongeza katika Kanuni ya Maadili ya Ulinzi wa Mtoto, pamoja na mabadiliko ya utaratibu wa kuripoti.
Februari 2021	2.5	Imepitiwa na So They Can

		International, hakuna mabadiliko yaliyofanywa, na maoni yameombwa kutoka ofisi za nchi husika.
Juni 2023	2.6	Imepitiwa na So They Can ina michango kutoka kwa Washirika wa Utekelezaji wa Programu wa So They Can, na marekebisho madogo yamefanywa.
Januari 2024	2.7	Kiambatisho F kimefanyiwa marekebisho – masharti ya uchunguzi: sharti la Cheti cha Kufanya Kazi na Watoto limeondolewa, na kipengele cha umri maalum kwa wageni wa muda mfupi kimeongezwa.
Novemba 2024	2.8	Kuwianisha Kanuni ya Maadili ya Ulinzi wa Mtoto na Kanuni ya Mwenendo wa Kitaaluma/ Kanuni ya Maadili ya Ulinzi wa Mtoto ya DFAT, pamoja na mapitio ya sera kila baada ya miaka miwili.
Oktoba 2025	2.8	Kuongeza So They Can England & Wales kwenye dibaji.
Februari 2026	2.9	Mapitio ya sera kuwianisha sera ya Ulinzi wa Mtoto ya DFAT CPP, Septemba 2025.

Kiambatisho A

KANUNI ZA MAADILI YA ULINZI WA MTOTO ZA SO THEY CAN

Wawakilishi wa So They Can kila wakati watahakikisha usalama na ulinzi wa watoto. Kipekee, Wawakilishi watapaswa:

- Kuwaheshimu watoto wote
- Kutotumia lugha au tabia isiyo sahihi kwa watoto, ikiwamo unyanyasaji, kuwatisha, udhalilishaji, ishara za kingono, kutofanya matendo yasiyoruhusiwa kiutamaduni

- Kutohusisha watoto walio chini ya umri wa miaka 18[1] katika aina yoyote ya vitendo vya kingono[2] au shughuli za kingono[3], ikiwamo kulipwa kwa ajili ya shughuli za kingono.

- Pale, inapowezekana, hakikisha kuna mtu mzima mwingine unapofanya kazi karibu na watoto.
- Kutokaribisha watoto wasio na mwangalizi kuingia katika makazi binafsi, isipokuwa wanakaribia kupatwa na hatari au wapo katika hatari.
- Kutolala karibu na watoto wasio na mwangalizi isipokuwa ni lazima sana, na katika hali yoyote ruhusa ya msimamizi lazima ipatikane, na ihakikishwe kuna mtu mzima mwingine kama inawezekana (kumbuka kuwa hili halihusishi watoto wa mtu binafsi).
- Kutotumia kompyuta yoyote, simu za mkononi, kamera za video, kamera za picha au mitandao ya kijamii kumdhalilisha au kumtisha mtoto, au kupata nyaraka za udhalilishaji wa watoto kupitia njia yoyote.
- Kutotoa adhabu za kimwili kwa watoto
- Kutoajiri watoto kwa kazi za nyumbani au kazi nyinginezo ambazo si sahihi kutokana na umri wao au hatua yao ya ukuaji; ambazo zinavuruga muda wao wa elimu na shughuli za burudani; au ambazo zinawaweka katika hatari kubwa ya kujeruhiwa.
- Kufuata sheria zote zinazohusika za Australia na za nchi husika, ikiwamo sheria za kazi zinazohusu ajira kwa mtoto.
- Kuripoti haraka tatizo au tuhuma za udhalilishaji unyanyasaji wa mtoto, na kutofuata sera kwa mujibu wa taratibu zinazofaa.
- Kueleza haraka mashtaka yote, hukumu na matokeo mengine ya kosa lolote linalohusiana na udhalilishaji na unyanyasaji wa watoto, ikiwamo yale yaliyo chini ya sheria za nchi, yaliyojiri kabla au wakati wa ushirikiano na DFAT.
- Kuwa makini na tabia na epuka vitendo au tabia ambazo zinaweza kuonekana na wengine kama udhalilishaji au unyanyasaji wa watoto.
- Tabia hizi hazikusudii kuingilia kati uhusiano wa kawaida ya familia.

Wakati wa kupiga picha au kurekodi video ya mtoto katika mradi wa So They Can, au kutumia picha za watoto kwa madhumuni yanayohusiana na kazi, wawakilishi wote au wapiga picha wa kujitegemea waliothibitishwa na So They Can lazima wafuate kikamilifu Miongozo ya Upigaji Picha wa Kimaadili ya So They Can kama ilivyo katika Kiambatanisho D, na ni lazima:

- kuhakikisha kuwa mila, desturi au masharti ya eneo husika yanaheshimiwa kabla ya kupiga picha au kurekodi video ya mtoto
- kupata ridhaa ya taarifa kutoka kwa mtoto na mzazi au mlezi wa mtoto kabla ya kupiga picha au kurekodi video. Maelezo kuhusu jinsi picha au video itakavyotumika lazima yatolewe.
- kuhakikisha picha, filamu, video na DVD zinawaonesha watoto kwa heshima na utu, na si kwa namna ambayo inawaweka katika hali ya hatari au chini ya udhalilishaji. Watoto wanapaswa kuvaa vizuri na kutokuwa katika makao unaoonekana kama za kingono.

[1] Ambapo mtoto ana umri wa miaka 16 au zaidi na upande mwingine hana zaidi ya miaka 2, na inaweza kuthibitishwa kuwa mtoto alikubali uhusiano huo, upekee unaweza kurekodiwa haraka katika mafaili ya wafanyakazi.

[2] Kama ilivyofafanuliwa chini ya Sheria ya Makosa ya Jinai, 1995.

[3] Kama ilivyofafanuliwa chini ya Sheria ya Makosa ya Jinai, 1995.

- kuhakikisha picha zinawakilisha kwa uaminifu muktadha na ukweli wa hali iliyopigwa
- kuhakikisha lebo za faili, meta data au maelezo ya maandishi hayafichui taarifa za utambulisho wa mtoto wakati wa kutuma picha kielektroniki au kuchapisha picha kwa njia yoyote

Kiambatisho B

Tamko la Kuzingatia Sera ya Ulinzi wa Mtoto ya So They Can

Mimi _____, ninakiri kwamba nimesoma na kuelewa nyaraka zifuatazo za So They Can.

- Sera ya Ulinzi wa Mtoto, na
- Kanuni za Maadili ya Ulinzi wa Mtoto

na ninakubali kwamba, katika kipindi chote cha ushirikiano wangu na So They Can, nitatekeleza na kuzingatia sera na Kanuni ya Maadili.

Saini: _____

Tarehe: _____

Baruapepe/namba ya simu: _____

Kiambatisho C

Tamko la Kuzingatia Kanuni za Maadili za Ulizi wa Mtoto za So They Can
(kwa wageni wa muda mfupi, wasambazaji, na wafanyakazi wa muda)

Mimi _____, ninakiri kwamba nimesoma na kuelewa Kanuni za Maadili ya Ulinzi wa Mtoto za So They Can

na ninakubali kwamba, katika kipindi chote cha ushirikiano wangu na So They Can, nitatekeleza na kuzingatia na Kanuni ya Maadili

Saini: _____

Tarehe: _____

Baruapepe/namba ya simu: _____

Kiambatisho D

MWONGOZO WA UPIGAJI PICHA KIMAADILI

Picha na video zinazopigwa na wafanyakazi wa So They Can au mpiga picha aliyeteuliwa na So They Can zinapaswa kuheshimu utu wa binadamu na kuhakikisha haki, usalama na ustawi wa mtu au watu wanaooneshwa. Hii ina maanisha:

- kuzingatia mila za eneo husika au vikwazo vinavyohusu upigaji au uzalishaji wa picha za watu, vitu au maeneo.
- kuelewa sheria za kitaifa zinazohusiana na upigaji picha, kurekodi video na haki za faragha
- kupata ridhaa sahihi ya maandishi au ya mdomo kabla ya kupiga picha au kurekodi video (ridhaa ya mdomo inakubalika, lakini lazima iandikwe na kuhifadhiwa kwa uwazi). Ridhaa ya kabla ina maana kwamba mtu anaelewa na anakiri kile anachotoa ridhaa yake.
- kueleza kwamba ridhaa inaweza kuondolewa wakati wowote, pamoja na kuelekeza namna ya kufanya hivyo, na kutoa taarifa kwamba kutokana na kudumu kwa maudhui ya mtandaoni, kuondoa ridhaa huenda mara zote kusiweze kusababisha kuondolewa kwa picha mtandaoni.
- kuheshimu haki ya mtu ya kukataa kupigwa picha au kurekodiwa video. Endapo utaona dalili zozote za kusita au kuchanganyikiwa, jiepushe kupiga picha au kurekodi video.
- kutosababisha madhara. Watu binafsi au makundi yanaweza kuwekwa katika hatari ya kulipiziwa kisasi, kufanyiwa vurugu au kukataliwa katika jamii zao kutokana na kufichuliwa kwa utambulisho wao au simulizi zao binafsi kupitia uchapishaji wa picha au urushaji wa video zao.
- kutowasilisha taarifa kwa upotoshaji kuhusu mtu, hali, muktadha na eneo la picha au video
- hairuhusiwi kabisa kutoa malipo au aina yoyote ya fidia kwa wahusika kama mbadala wa kupigwa picha au kurekodiwa video, au kwa ajili kupata ridhaa au saini yao ya ruhusa ya kuchapishwa au kurushwa hewani.

Picha na video zinazohusu masuala nyeti ya kiutamaduni, kisiasa au ya unyanyapaa kijamii lazima zilinde utambulisho na faragha ya wahusika.

- Zisitambulishe mhusika. Weka kamera kwa namna ambayo nyuso na sifa nyingine za kipekee haziwezi kutambuliwa.
- Pata ridhaa ya maandishi kabla ya kutumia majina halisi na maeneo katika mazingira ambayo kufichuliwa kunaweza kusababisha madhara. Vinginevyo, ondoa taarifa binafsi kama vile majina na maeneo kwenye maelezo ya picha au nyaraka nyingine zozote zinazohusiana.
- Picha zinazoweza kumtambulisha mhusika hazipaswi kutumiwa kuwasilisha masuala nyeti kwa namna inayodokeza kwamba mtu huyo anahusishwa na suala husika.
- Waathirika walionusurika katika udhalilishaji wa kingono, ukatili wa kijinsia au unyanyasaji hawapaswi kutambuliwa au kuonyeshwa.

Picha au video za watu wenye mahitaji maalum zinapaswa kupigwa kwa uangalifu wa hali ya juu, huruma, na kwa kulinda faragha zao.

- Piga picha au rekodi video za watu wote kwa heshima na utu. Umakini wa kipekee na huruma vinapaswa kuzingatiwa kwa watu walio katika mazingira hatarishi.
- Hali ya mtu kuishi na VVU, kifuakikuu au hali nyingine yoyote nzito ya kiafya haitapaswa kufichuliwa bila kupata ridhaa ya maandishi kabla.
- Ushiriki wa mtu katika biashara ya ngono au shughuli nyingine zinazopingwa kijamii au zinazochukuliwa kuwa za kihalifu (au ni uhalifu) hautapaswa kutambuliwa.
- Tahadhari ichukuliwe wakati wa kupiga picha au kurekodi video za watu katika nyakati za misukosuko. Usitumie au kunufaika na hali ya udhaifu wa mtu wakati wa matatizo au huzuni.

Picha au video za watoto zinazopigwa kwa madhumuni yanayohusiana na kazi lazima zizingatie viwango vinavyotokana na Sera ya Ulinzi wa Watoto ya So They Can. Kabla ya kupiga picha au kurekodi video ya mtoto, wafanyakazi au wenye mkataba lazima wapate ridhaa ya maandishi kutoka kwa mtoto na mzazi au mlezi, na kueleza jinsi picha au video itakavyotumika. Katika mazingira ya makundi kama darasa, uthibitisho wa ridhaa ya awali ya mzazi unapaswa kupatikana kutoka kwa mkuu wa shule au mwalimu mkuu. Pia:

- kabla ya kupiga picha au kurekodi video ya mtoto, tathmini na zingatia sheria za eneo, mila au masharti yanayohusu uzalishaji wa picha.
- hakikisha picha na video zinaonyesha watoto kwa heshima na utu, na sio katika hali za udhaifu au udhalilishaji. Watoto wanapaswa kuvaa vizuri na wasiwe katika mwonekano unaoweza kuashiria tabia za kingono.
- kamwe usitumie picha za mtoto aliyefariki au aliye katika mateso makubwa bila ishara yoyote ya msaada ulio karibu
- fikiria kuweka alamabainishi (*watermark*) kwenye picha ya mtandaoni ili kuzuia matumizi mabaya
- picha lazima ziwakilishe ukweli wa muktadha na matukio
- majina ya mafaili hayapaswi kufichua taarifa zinazoweza kumtambua mtoto wakati wa kutuma picha au video kwa njia ya kielektroni

KIELELEZO E

FOMU YA TAARIFA YA TUKIO LA ULINZI WA MTOTO

Tukio lilitopea wapi?

Muda: _____Tarehe: _____Mahali: _____

Taarifa za Mtoataarifa:

Jina: _____Anwani:

_____Namba ya simu (na baruapepe kama inawezekana):

_____

Kazi: _____ Uhusiano na Mtoto: _____

Taarifa za Mtoto:

Jina:

_____

Anwani:

_____

Umri: _____ Tarehe ya kuzaliwa: _____ Jinsia:

_____

Muundo wa Kaya:

_____

Kabila: _____ Dini:

_____

Ulemavu wowote:

_____

__

Shule: _____ Darasa: _____

Mwalimu: _____

Taarifa za Tukio:

_____

_____

_____

_____

Maelezo ya tatizo (ikiwamo maelezo ya mtoto kama inawezekana):

_____

_____

_____

_____

Mabadiliko yoyote katika tabia ya mtoto:

_____

_____

_____

_____

Taarifa za Mshukiwa:

Jina:

_____

_____

Anwani:

_____

_____

Namba ya simu:

_____

Hali ya sasa ya usalama wa mtoto:

_____

Vipimo vya kitabibu vimefanyika? Ndiyo/Hapana Kama vimefanyika:

Jina la tabibu:

_____

Mawasiliano ya tabibu

_____

Tarehe ya vipimo (tafadhali ambatisha ripoti):

_____

_____

Ni nani mwingine anajua?

_____

Hatua iliyochukuliwa hadi sasa:

_____

_____

Hatua zinazofuata:

_____

_____

_____

_____

Ripoti imeandaliwa na: _____Tarehe: _____

Imesainiwa na: _____Tarehe: _____

Fomu zote za taarifa za Tukio la Ulinzi wa Mtoto lazima zitumwe kwa baruapepe kwa Kitengo cha Maadili na Tabia **cha DFAT kwa anwani childprotection@dfat.gov.au**.

Kiambatisho F

Masharti ya uchunguzi wa ulinzi wa mtoto ya So They Can

Wawakilishi wa So They Can	**Masharti ya uchunguzi wakati wa kuajiriwa**	**Jukumu**
Wajumbe wa Bodi ya So They Can na Wawakilishi walioko Australia, New Zealand na Marekani wasio na mawasiliano ya moja kwa moja na watoto.	Ripoti ya Rekodi ya Uhalifu ya Jeshi la Polisi la Shirikisho la Australia**,** Jeshi la Polisi la New Zealand au Idara ya Huduma za Taarifa za Haki ya Jinai ya FBI (Marekani (kama inavyotakiwa), kilichotolewa na nchi husika ndani ya kipindi cha miezi 12 au chini ya hapo kabla ya uteuzi. Iwapo mtu huyo amekuwa akiishi nje ya nchi husika ya utekelezaji wa programu, basi ukaguzi wa rekodi ya uhalifu lazima ufanywe kwa kila nchi aliyokaa kwa kipindi cha miezi 12 au zaidi katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita, pamoja na nchi ya uraia wa mtu huyo. Tamko lililosainiwa la kuthibitisha kufuata Sera ya Ulinzi wa Mtoto ya So They C	CEO, CFO
Wajumbe wa Bodi ya So They Can na Wawakilishi walioko Australia na New Zealand wasio na mawasiliano ya moja kwa moja na watoto.	Ripoti ya Ukaguzi wa rekodi ya uhalifu kutoka Jeshi la Polisi la Shirikisho la Australia, Jeshi la Polisi la New Zealand au Idara ya Huduma za Taarifa za Haki ya Jinai ya FBI nchini Marekani (kulingana na nchi husika), uliofanyika ndani ya kipindi cha miezi 12 au chini ya hapo kabla ya uteuzi. Iwapo mtu huyo amekuwa akiishi nje ya nchi husika ya utekelezaji wa programu, ukaguzi wa rekodi ya uhalifu lazima ufanywe kwa kila nchi aliyokaa kwa muda wa miezi 12 au zaidi katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita, pamoja na nchi ya uraia wa mtu huyo. Tamko lililosainiwa la kuthibitisha kufuata Sera ya Ulinzi wa Mtoto ya So They Can	CEO, CFO, Meneja wa Wanaojitolea wa So They Can

Wawakilishi wa So They Can wenye umri wa miaka 16 na zaidi katika nchi za utekelezaji wa programu wenye mawasiliano ya moja kwa moja na watoto.	Ripoti ya Ukaguzi wa rekodi ya uhalifu unaotolewa na mamlaka ya polisi ya eneo husika katika nchi ya utekelezaji wa programu, uliofanyika ndani ya kipindi cha miezi 12 au chini ya hapo kabla ya uteuzi. Iwapo mtu huyo amekuwa akiishi nje ya nchi husika ya utekelezaji wa programu, ukaguzi wa rekodi ya uhalifu lazima ufanywe kwa kila nchi aliyokaa kwa muda wa miezi 12 au zaidi katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita, pamoja na nchi ya uraia wa mtu huyo. Tamko lililosainiwa la kuthibitisha kufuata Sera ya Ulinzi wa Mtoto ya So They Can.	CEO, Meneja wa Wanajitolea wa So They Can, na Wakurugenzi wa Nchi wa So They Can
Wawakilishi wa So They Can wenye umri wa miaka 16 na kuendelea katika nchi za utekelezaji wa programu wanaofanya kazi na watoto.	Ukaguzi wa rekodi ya uhalifu unaofanywa na mamlaka ya polisi ya eneo husika katika nchi ya utekelezaji wa programu ikiwa upo. Ukaguzi huu lazima uwe umefanyika ndani ya kipindi cha miezi 12 au chini ya hapo kabla ya uteuzi. Iwapo mtu huyo amekuwa akiishi nje ya nchi husika ya utekelezaji wa programu, ukaguzi wa rekodi ya uhalifu lazima ufanywe kwa kila nchi aliyokaa kwa muda wa miezi 12 au zaidi katika miaka mitano (5) iliyopita, pamoja na nchi ya uraia wa mtu huyo. Tamko lililosainiwa la kuthibitisha kufuata Sera ya Ulinzi wa Mtoto ya So They Can. Mafunzo ya ziada na maalum na endelevu ya ulinzi wa mtoto kulingana na kazi. Mipango ya usaili inayojumuisha maswali ya kitabia yanayohusiana na nafasi zinazohusisha kufanya kazi na watoto. Ukaguzi wa uhakiki unaofanyika wakati Wawakilishi wanapokuwa na mabadiliko ya hali au mazingira.	CEO, Meneja wa Wanaojitolea wa So They Can, Wakurugenzi wa Nchi wa So They Can, na Wasimamizi wa Miradi.

Wawakilishi wa So They Can wenye umri wa miaka 16 na kuendelea katika nchi za utekelezaji wa programu wasio na mawasiliano ya moja kwa moja na watoto.	Ukaguzi wa rekodi ya uhalifu unaofanywa na mamlaka ya polisi ya eneo husika katika nchi ya utekelezaji wa programu – ikiwa upo, uliofanywa ndani ya kipindi cha miezi 12 au chini ya hapo kabla ya uteuzi. Iwapo mtu huyo amekuwa akiishi nje ya nchi husika ya utekelezaji wa programu, ukaguzi wa rekodi ya uhalifu lazima ufanywe kwa kila nchi aliyokaa kwa muda wa miezi 12 au zaidi katika miaka mitano (5) iliyopita, pamoja na nchi ya uraia wa mtu huyo. Tamko lililosainiwa la kuthibitisha kufuata Kanuni ya Maadili ya Ulinzi wa Mtoto ya So They Can.	CEO, Meneja wa Wanaojitolea wa So They Can, Wakurugenzi wa Nchi, Wasimamizi wa Miradi.
Wageni wa muda mfupi wa kawaida na wafanyakazi wa muda ambao hawafanyi kazi na watoto.	Tamko lililosainiwa la kuthibitisha kufuata Kanuni ya Maadili ya Ulinzi wa Mtoto ya So They Can kuanzia umri wa miaka 16.	Wasimamizi wa Mradi

Mbali na uchunguzi mahususi unaohitajika kwa madhumuni ya ulinzi wa watoto, taratibu za tathmini na uteuzi wa kina zinapaswa kutumika, zikiwamo (lakini bila kikomo kwa):

- Maelezo ya kina ya kazi na vigezo vya uteuzi.
- Usaili wa kina ya uteuzi, ikiwa ni pamoja na maswali yanayohusiana na kazi na watoto.
- Ukaguzi wa wadhamini, ikiwa ni pamoja na maswali kuhusu ufanisi na uwezo wa kufanya kazi na watoto.
- Uhakiki wa nyaraka.
- Kipindi cha maelekezo ya kazi chenye ufuatiliaji, usimamizi na mapitio rasmi.

Kiambatisho G

Viwango vya Ulinzi wa Mtoto kwa Washirika wa DFAT

Viwango	Msingi	Jumuishi
1. Sera na taratibu za ulinzi wa watoto, zikiwamo Kanuni ya Maadili	Shirika lina sera/taarifa ya ulinzi wa watoto au nyaraka za sera na taratibu zingine ambazo zinakidhi matarajio ya Sera ya Ulinzi wa Watoto ya DFAT. Shirika lina Kanuni ya Maadili inayolingana na Kanuni ya Maadili ya Ulinzi wa Watoto ya DFAT. Wafanyakazi wote wanapaswa kuthibitisha kwamba wamesoma na wamekubali Kanuni ya Maadili ya shirika. Washirika wanahimizwa kuandaa sera, taratibu na kanuni zao zinazohusiana na ulinzi wa watoto, lakini wanaweza pia kutumia sera za mshirika wao mkuu (So They Can). Wafanyakazi wote wanahitajika kuthibitisha kwamba wamesoma na wamekubali Kanuni ya Maadili ya shirika. Washirika wanahimizwa kuandaa sera, taratibu na kanuni zao maalum za ulinzi wa watoto, lakini wanaweza pia kutumia sera za mshirika wao mkuu (So They Can) kama inafaa.	Shirika lina sera na taratibu za jumuishi za ulinzi wa watoto ambazo zinakidhi matarajio ya Sera ya Ulinzi wa Watoto ya DFAT na zinakaguliwa mara kwa mara. Sera hiyo inapaswa kuonyesha ahadi ya shirika ya kutovumilia unyonyaji, unyanyasaji na madhara kwa watoto, na kuweka taratibu zinazolingana na viwango hivi. Shirika lina Kanuni yake ya Maadili inayolingana na Kanuni ya Maadili ya Ulinzi wa Watoto ya DFAT. Wafanyakazi wote wanahitajika kuthibitisha kwamba wamesoma na wamekubali Kanuni ya Maadili ya shirika. Washirika wanahimizwa kuandaa sera, taratibu na kanuni zao maalum za ulinzi wa watoto, lakini wanaweza pia kutumia sera za mshirika wao mkuu (So They Can) ikiwa inafaa.
2. Njia za Kuripoti na Taratibu za Uchunguzi	Shirika linaweza kupokea na kusimamia taarifa za matukio kwa usalama na kwa usiri, kwa mujibu wa sheria za Australia na/au za eneo husika. Njia za kuripoti zinapatikana kwa wadau wote, ikiwamo watoto. Shirika lazima liripoti matukio na matokeo ya uchunguzi kwa DFAT.	Shirika lina mfumo uliotangazwa vyema, unaopatikana kwa urahisi (ikiwa ni pamoja na kwa watoto), unaohakikisha usiri na usalama wa kuripoti tatizo au matukio ya ulinzi wa watoto, pamoja na ulinzi dhidi ya hatua za kulipiza kisasi. Shirika lina nyaraka za taratibu za kusimamia matukio ya ulinzi wa watoto zinazojumuisha majibu yanayozingatia athari za kiakili na kisaikolojia, taratibu za usawa, michakato ya uchunguzi iliyo wazi na ya wakati, ulinzi wa faragha, msaada kwa watoto walioathirika, na hatua za kinidhamu zinazofaa ikiwa tukio linahusisha wafanyakazi wake. Shirika linahakikisha kuwa watoto, familia na jamii wanapewa taarifa kuhusu tabia zinazotarajiwa, njia za kuripoti na michakato ya uchunguzi kwa njia

Viwango	Msingi	Jumuishi
		zinazopatikana kwa urahisi na zinazofaa kiasili. Shirika lazima liripoti matukio na matokeo ya uchunguzi kwa DFAT.
3. Taratibu za Usimamizi wa Vihatarishi	Shirika linafanya tathmini ya vihatarishi vya ulinzi wa watoto, ikijumuisha hatua za kupunguza vihatarishi kulingana na shughuli na muktadha husika, ambayo inafanyiwa mapitio angalau mara moja kwa mwaka na kurekebishwa inapohitajika.	Shirika linafanya tathmini ya vihatarishi vya ulinzi wa watoto, ikijumuisha hatua za kupunguza vihatarishi kulingana na shughuli na muktadha husika, ambayo inafanyiwa mapitio angalau mara moja kwa mwaka na kurekebishwa inapohitajika. Shirika lazima liwe na ushahidi wa maandishi unaoonyesha kwamba uongozi wa juu na bodi za utendaji wanafuatilia usimamizi wa vihatarishi vya ulinzi wa watoto. Shirika lina ushahidi wa maandishi wa matarajio yake kwa washirika wake na jinsi washirika hao watakavyosimamia vihatarishi vya ulinzi wa watoto.
4. Mafunzo ya Ulinzi wa Watoto	Shirika linatoa mafunzo ya msingi ya ulinzi wa watoto kwa wafanyakazi wote wanaohusika. Wafanyakazi wanahitajika kukamilisha mafunzo hayo kila mwaka.	Shirika linatoa mafunzo ya jumuishi kwa wafanyakazi wote ya ulinzi wa watoto yanayofanyiwa mapitio mara kwa mara. Wafanyakazi wanahitajika kukamilisha mafunzo hayo kila mwaka.
5. Taratibu za Ajira na Uchunguzi za Usalama wa Mtoto	Shirika linatekeleza ajira salama kwa watoto na uchunguzi wa uadilifu kwa wafanyakazi wote. Uchunguzi unapaswa kujumuisha ukaguzi wa wadhamini, ukaguzi wa hivi karibuni wa polisi, ukaguzi wa kufanya kazi na watoto au watu walio katika mazingira hatarishi, au ukaguzi mbadala unaofaa kwa eneo husika, au pale ambapo haya haywezekani, tamko la binafsi.	Shirika linatekeleza ajira salama kwa watoto na uchunguzi wa uadilifu kwa wafanyakazi wote. Uchunguzi unapaswa kujumuisha ukaguzi wa wadhamini, ukaguzi wa hivi karibuni wa polisi, ukaguzi wa kufanya kazi na watoto au watu walio katika mazingira hatarishi, au ukaguzi mbadala unaofaa kwa eneo husika, au pale ambapo haya hayawezekani, tamko la binafsi. Hatua za ziada za uadilifu zinahusisha ujumbe na maswali maalumu kuhusu ulinzi wa watoto katika hatua zote za ajira na kuajiriwa, pamoja na ufuatiliaji endelevu wa tabia za wafanyakazi na utekelezaji wa sera na taratibu za ulinzi wa watoto.